LIC LOCAL INVESTMENT CLIMATE

**Brief No. 9**

# PROGRAMU YA USIMAMIZI WA ARDHI (DODOMA NA KIGOMA)

Mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) ni mradi wa kuendeleza sekta binafsi unaofadhiliwa na Danida. Mradi unashughulikia vikwazo vikuu vinavyokwamisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya wilaya kwenye mikoa miwili ya Dodoma na Kigoma nchini Tanzania. LIC imejikita katika mijadala kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miundombinu ya utoaji wa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na vituo vya pamoja vya biashara na miundombinu ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji. Washirika wanaotekeleza mradi wa LIC ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretariati za mikoa ya Kigoma na Dodoma, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Tanzania, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

**Malengo ya mradi wa usimamizi ardhi ni:**

i. Kuanzisha mfumo endelevu wenye gharama nafuu na unaotumia muda kiufanisi katika kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini na utolewaji wa hati za kimila pamoja na utoaji wa hati za kawaida katika sehemu za mijini.
ii. Kujenga uwezo wa serikali za mtaa kuandaa mipango wa matumizi bora ya ardhi vijijini na kutoa hati za kimila
iii. Kuanzisha kanzi data (central database) ambayo ni rafiki kwa mtumiaji katika kusaidia mpango wa matumizi bora ya ardhi vijijini, utoaji wa hati za kimila na hati za kawaida.
iv. Kuongeza uelewa wa jamii kuhusu, umuhimu wa mipango ya matumizi bora ya ardhi na hati miliki za kuwajengea uwezo wataalamu wa Ardhi kuanzia ngazi ya vijiji mpaka ngazi ya wilaya
v. Kutengeneza mfumo ambao utaweza kutumika katika Halmashauri nyingine



Shamba la mpunga, Mtazamo katika wilaya ya Bahi



Miundombinu ya umwagiliaji, Matajira

Kufikia malengo yaliyotajwa hapo juu, mradi wa LIC umeandaa mfumo utakaowezesha kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi endelevu, wa gharama nafuu na kwa haraka ambao unajumuisha utoaji wa hati za kimila katika vijiji vitatu vilivyo jirani bila kuathiri mamlaka ya vijiji shiriki au kukengeuka miongozo iliyowekwa na Tume ya Mipango Bora ya Matumizi ya Ardhi ya Taifa(NLUPC).



Shamba la miti ya miembe, Dodoma



Makabidhiano ya hati za kimila CCROs kwa wamiliki wa mashamba ya maembe katika kijiji cha Chifukulo, Dodoma

Mfumo huu hautoi tu suluhisho ya migogoro ya mipaka, lakini pia unaokoa muda na kupunguza gharama kwa karibu asilimia 50 ikilinganishwa na njia za kawaida. Mfumo huu pia unatoa ufumbuzi wa changamoto ya ukosefu wa fedha ndani ya serikali za mtaa katika kuandaa hati za kimila (CCROs) na hati za kawaida (CROs) kwa kuanzisha Mfuko Maalumu wa Usimamizi wa Ardhi kupitia SPV ambazo zimeanzishwa ndani ya Halmashauri kwa lengo la kusimamia masuala ya ardhi.

Maeneo ya mjini, serikali za mtaa kupitia SPV wanaweza kupata ardhi, kuipima na kupata viwanja vyenye hati na hatimaye kuviuza. Katika maeneo ya vijijini, ambapo Sheria ya Ardhi ya Viiji iinatumiaka, SPV inafanya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji na kutoa Hati za Kimila kupitia mfumo wa kuchangia gharama ambapo mmiliki wa ardhi anachangia kuanzia Shilingi 50,000/= mpaka 90,000/= kwa kitalu kutokana na idadi ya vitalu anavyomiliki. Njia hii itaboresha sana mfumo na utaratibu za utoaji ardhi kwa wafanyabiashara na wanawake na mfumo huu unaweza kuigwa na serikali za mtaa zote nchini Tanzania.

Mbali zaidi, katika kutambua ukweli kwamba moja ya kizuizi kikubwa kwa wafanyabiashara kupata mikopo ni kukosekana kwa hati miliki za ardhi , LIC itaendelea kufanya kazi na mamlaka za serikali husika na wadau wa sekta ya fedha pamoja na wafanyabiashara kuelezea changamoto za kisheria na kiutawala katika usimamizi ardhi Tanzania, haswa ardhi ya vijiji.

## Mambo muhimu na matarajio

Kusudi Kubwa la mradi wa LIC katika Usimamizi wa Ardhi ni kuacha mfumo endelevu wa usimamizi wa matumizi bora ya Ardhi ambao ni endelevu. Mfumo huu ulioelezewa hapo juu unajaribiwa katika mikoa ya Dodoma na Kigoma na inatarajiwa kwamba kufikia mwishoni mwa mwaka 2019 zaidi ya hati miliki za kawaida 5,000 na hati miliki za kimila 15,000 zitakuwa zimetolewa.

Inategemewa kwamba msaada wa programu ya ardhi kutoka LIC utaongeza uwezo wa serikali za mtaa katika kusimamia utoaji wa hati hivyo kuboresha mazingira ya uwekezaji katika ngazi ya Wilaya. Mbali zaidi, inategemewa kwamba mfumo huu wa LIC wa Usimamizi wa Ardhi utatatua changamoto kubwa ya kifedha inayoikumba serikali za mitaa kwenye usimamizi wa ardhi.

Mfumo wa usimamizi wa ardhi wa mradi wa LIC kwa sasa unatekelezwa katika Wilaya ya Chamwino, Kongwa, Kondoa na Bahi mkoani Dodoma na wilaya ya Kasulu, Uvinza na Kibondo mkoani Kigoma. Wadau wengine katika utekelezaji wa program hii ni pamoja na Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi, Halmashauri za Wilaya, washauri binafsi, wafanyabiashara wake kwa waume pamoja na vyama vya wakulima. Wilayani Uvinza pekee zaidi ya mashamba/viwanja 2,500 zimeshapimwa na hati za kimila kuandaliwa mnamo mwezi wa kwanza 2019.

Shughuli zinazoendelea zinajumuisha kukusanya taarifa za lazima zitakazo saidia kuandaa kanzi data (database) katika kusaidia mpango wa matumizi bora ya ardhi vijijini, utoaji wa hati za kimila na hati za kawaida. Mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini na kuanzishwa kwa zoezi la kuandikisha ardhi kwenye zaidi ya vijiji 25 vya majaribio vitamalizika mwaka 2019.

LIC tayari imewekeza zaidi ya Shilingi za Tanzania Milioni 700 katika matumizi bora ya ardhi na kuendeleza kanzi data katika mikoa ya Dodoma na Kigoma.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya mradi wa LIC: www.lic.or.tz

**Januari 2019**